ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tano – Tarehe 25 Januari, 2011

*Kikao kilianza Saa 3:00 asu*buhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 20

Utoaji wa Daftari la Kudumu kwa Vyama vya Siasa

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inafanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya 1984. Kwa kuwa Tume hii katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 ilitoa Daftari la Kudumu la Wapiga kura kwa vyama vya siasa kabla ya uchaguzi mkuu.

Je, Mhe. Waziri ni sheria na kifungu gani cha Sheria kilichotumiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya kutoa daftari la wapiga kura kwa vyama vya siasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sheria iliyotumika kutoa nakala za Daftari la Wapiga Kura kwa vyama vya siasa ni Sheria Nam. 11 ya 1984, kifungu Nam. 13(8) cha Sheria hiyo. Kifungu hiki cha 113(8) cha Sheria Nam. 11 ya 1984 kinatoa uwezo kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutayarisha Kanuni zinazohusu namna ya uwekaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, idadi ya madaftari hayo, matumizi yake ya namna ya kuweka pingamizi.

Kwa kutumia mamlaka hiyo ya kisheria, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imetayarisha Kanuni za Ukaguzi wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2010, kifungu cha 9(3) cha Kanuni hizo kinaipa uwezo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutoa nakala ya Daftari ya Kudumu la Wapiga Kura kwa vyama vya Siasa. Mhe. Spika, Kanuni za Ukaguzi wa Daftari la Kudumu la

Wapiga Kura za mwaka 2010 zimechapishwa katika Tangazo Nam. 8 uk. 11 – 17 wa Gazeti Rasmi la Serikali CXIC NAM. 6363 la tarehe 30 Mei, 2010.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama alivyojibu Mhe. Waziri juu ya vifungu vilivyotoa nafasi au kanuni zilizotoa nafasi kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi kutoa daftari la uchaguzi kwa wapiga kura.

Mhe. Spika, fursa hii ilitumika vibaya kwa baadhi ya wana siasa kuwafuata waliojiandikisha kupiga kura na kuwatisha kuwa wasiende kupiga kura au vyenginevyo watakiona. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba iko haja ya kubadilisha kifungu hiki na kukiandika vyenginevyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nia ya kutunga sheria na nia ya kuweka kanuni ni kwa ajili yakutumia vizuri fursa zilizopo ili ziwezeshe kwa mujibu wa katiba na demokrasia, watu wetu waweze kuwa na haki ya kushiriki vizuri katika chaguzi zetu. Kama kipengele hiki kina tatizo lolote katika kukwamisha utaratibu huu tutashauriana na tume tuone kama kuna tatizo basi tuweze kurekebisha kwani nia yetu Mhe. Spika, ni kwamba uchaguzi ufanyike vizuri na kila mmoja apate haki yake. Mhe. Spika, kama kuna watu wanaitumia vibaya basi tutatafuta namna yoyote ile lakini kwanza lazima tufanye tathmini ili tuone kama yapo mapungufu hayo.

Mhe. Abdalla Juma Abdall: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa siku moja karibu na uchaguzi nilimsikia Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi akisema kwamba kuna watu katika daftari la kudumu la wapiga kura wameandikishwa mara mbili mbili.

Je, watu wale kwakuwa waligunduliwa walichukuliwa hatua gani na sasa wadau wa uchaguzi watapata fursa wakati gani wakuweza kuhakikisha kama wale watu wameondolewa katika daftari.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nia kubwa ya Tume ya Uchaguzi kupitia sheria na kanuni zake ni kuhakikisha kwamba uchaguzi unafanyika vizuri kidemokrasia na kila mmoja anapata haki yake ya kikatiba. Yanapotokea mapungufu tume yetu huchukua kila hatua kurekebisha mapungufu hayo na kwa sababu wananchi sasa ningependa yale marekebisho yaliyotokea wayajue kwa undani na kwa kina zaidi, kwani tutashauriana na tume kwa mujibu wa uwezo iliyonayo ili wachukue hatua zinazofaa yote wanayoyafanya yawe kwa uwazi na watu wote waweze kuridhika na hatua hizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni sawa na tume nyengine za kilimwengu yaani zinatakiwa ziendeshe uchaguzi uliokuwa huru na wa haki na kuhakikisha kwamba kila aliyekuwa na haki ya kupiga kura anapata kupiga kura.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna Wazanzibari wengi ambao katika uchaguzi mkuu uliopita walikosa nafasi yakupiga kura kwa uchaguzi wa Zanzibar na hatimae kupata kupiga kura ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tu.

a) Je, ni lini wale Wazanzibari ambao wamekosa haki zao za kupiga kura ya Zanzibar ambao wamekidhi matakwa yakuwa wapiga kura ya Zanzibar wataingizwa katika daftari hili.

b) Je, isingekuwa vyema Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ikaliacha wazi daftari hili kila kipindi cha mwaka mmoja ili kutoa nakala kwa vyama vya siasa kuweza kujua ongezeko la wapiga kura kila baada ya mwaka.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali langu la msingi wiki iliyopita nilieleza wazi adhma ya tume kurekebisha kasoro mbali mbali zilizojitokeza katika uchaguzi uliopita kwa msingi kwamba chaguzi nyengine zote zitakazofanyika zifanyike vizuri zaidi.

Mhe. Spika, hata hivyo napenda nichukue fursa hii kuwapongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa namna walivyoendesha uchaguzi wetu mkuu uliopita kwa amani, utulivu mkubwa na vyama vyote vya siasa wakakubali matokeo hayo. Kwa hivyo, hizo lazima tuwape pongezi zao pia nilisema kwamba jitihada zitachukuliwa kuhakikisha kwamba kasoro zinazojitokeza zirekebishwe ili haki ya kila mmoja ipatikane.

Mhe. Spika, kuhusu daftari kuwa wazi ni kwamba ipo fomu maalum kwa mujibu wa kanuni zile na hapa ninao mfano unaweza kuitumia ili kupata nafasi ya kuona daftari lile kama lina kasoro yoyote. Haki hiyo wanaipata vyama vya siasa, haki hiyo pia wanaipata wananchi wote. Kwa hivyo, naona utaratibu uliopo ni mzuri, lakini kama Mhe. Mwakilishi anao utaratibu mwengine wowote mzuri zaidi ende aonane na Tume ya Uchaguzi ili nia yetu ni kufanya marekebisho yaliokuwa mazuri zaidi yawafae wananchi wetu katika visiwa vyetu hivi na mara zote tukifanya uchaguzi uwe wa amani, utulivu na upendo.

Nam. 90

Utunzaji wa Gari za Serikali

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Katika mzunguko wa barabara ya Michenzani (Round About) Serikali ilijenga bwawa lenye kurusha maji na kuleta haiba nzuri ya eneo hilo.

(a) Kwa kuwa hivi sasa bwawa hilo linaonekana kupoteza haiba yake. Je, kuna sababu zipi zilizopelekea kufeli kwa mpango wa awali.

(b) Je, hivi wizara haioni haja ya hulijaza eneo hilo kwa udongo na kuotesha bustani za kileo, kuliko kuliacha katika hali ile ya uchakavu na isiyofurahisha machoni mwa watu.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 90, (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, bwawa liliopo katika mzunguko wa barabara ya Michenzani *(Round about)* limesita kufanya kazi kwa sababu za kuharibika kwa mfumo mzima wa kurushia maji kulikotokana na kuharibika kwa pampu tatu, mtambo wa umeme *(Control panel),* nozeli za kurushia maji, taa maalum za rangi na kuvuja kwa sakafu ya bwawa hilo.

(b) Wataalamu wa Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Wataalamu wa Idara ya Majenzi walifanya juhudi kubwa za kulifufua bwawa hilo. Wataalamu hao wamekuja na ushauri wa aina tatu:-

(i) Kubadilisha mfumo wote wa kurushia maji na kuweka mwengine

(ii) Kubadilisha mfumo kwa kuweka nusu bustani na nusu mfumo wa urushaji maji.

(iii) Kuliondoa bwawa hilo na kuligeuza bustani.

Serikali inaendelea kuzingatia ushauri uliotolewa na wataalamu hao hasa baada ya kuonekana kwamba kubadilisha mfumo na kuweka mwengine utakuwa ni wa gharama kubwa (Tzs. 48,900,000/=) Hata hivyo, kipaumbele cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hasa kwa kuzingatia zile fikra za mzee wetu Abeid Amani Karume alipoliweka bwawa lile kati kati ya mji mpya ni kulifanyia matengenezo bwawa hilo bila ya kuharibu uasili wake.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi nataka kujua hasa ni nani mwenye mamlaka ya kuliendeleza bwawa lile kati ya Manispaa au Idara ya Majenzi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Idara ya Manispaa ndio dhamana wa masuala yote ya usafi, michirizi, bustani katika mji wetu huu wa Zanzibar wao ndio watizamaji na wasimamizi wa mambo yote yale. Lakini kitaaluma au kitaalamu kwa suala lile ni Idara ya Majenzi na wao ndio waliohusika hasa na uanzishaji na ujenzi wa bwawa lile. Kwa hivyo, kumbukumbu nyingi na mambo mengi yako idarani kule.

Mhe. Spika, kama nilivyosema suala la msingi ni kulifufua bwawa lile kwa hiyo inahitajika tushirikiane idara zote ili kupata taaluma, kupata utaalamu na kupata kila uwezekano na mbinu ya kulifufua bwawa lile. Kwa hivyo, tutashirikiana na kila taasisi hata binafsi ili watusaidie pengine kuna taaluma hatujaifahamu kuweza kulifufua bwawa lile.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa hoteli za kawaida tu zinayadumisha mabwawa kama hayo yenye kurusha maji, ni kwa kiwango gani serikali imezembea hata bwawa lile likafikia hadi kufa na sasa hivi linataka kufufuliwa.

b) Mhe. Spika, kwa kuwa Manispaa ndio inayotoa vibali vya matangazo mbali mbali barabarani vya mashirika ya simu ambayo matangazo hayo ni ghali na yameenea kila pahala. Je, hakuna utaratibu wowote wakuyachukua haya mashirika ya simu wakalifufua hili bwawa ili wakaweza kutoa matangazo yao kati kati ya mji.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba ni kweli mahoteli mengi yamekuwa na mabwawa yao na wanafanya kila jitihada za kuyaendeleza. Kwa kweli muda mwingi ulipopita sote tunafahamu matatizo yaliyotokezea ya maji na matatizo ya umeme katika kisiwa chetu cha Unguja. Kwa hivyo, matatizo yote hayo yaliyotokezea nasema ni mambo mengi yamechangia kufa kwa bwawa lile, sisemi suala moja.

Kwa hivyo, serikali imeona matatizo hayo na sasa tumejipanga upya kulitengeneza na kulifufua ili kurudisha haiba ya mji wetu. Kwa hivyo, halikutengenezwa wakati huo sio sababu la muhimu ni kujipanga ukaliona tatizo na ukalirekebisha, hilo ndio suala la msingi hivi sasa tumeshajipanga tutajitahidi ili lipendeze kabisa.

Mhe. Spika, pia ni kweli kuhusu wenye mabango ya simu wale ni kwamba wanaongeza haiba ya mji hilo ni jambo la kawaida katika miji yote mikubwa na ni ushindani wa biashara, la muhimu ni kwamba walipe mapato yetu na sisi hilo tunalifuatilia kama mtu halipi basi tunaliondoa. Mhe. Spika, ZANTEL waliwahi kutoa aidia hiyo kwamba na wao wangesaidia utengenezaji wa bwawa hilo, aidia hiyo bado tunaifuatilia tuone ukweli wake.

Nam. 35

Usambazaji wa Huduma ya Umeme

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Kwa kuzingatia kuwa Serikali imekuwa na mpango wa kuwasaidia wananchi pale ambapo wananchi hao wameanza kuonesha juhudi za kujiletea huduma muhimu kama za umeme katika maeneo yao.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa vijiji vya Mwane na Kivugo Kiungoni ambao tayari wamejitafutia nguzo kiasi ya kumi na tisa, ili kuwapelekea huduma ya umeme katika vijiji hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inatoa shukurani kwa wananchi wa vijiji ambavyo vinapenda kujiletea maendeleo katika vijiji hivyo. Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme inathamini sana michango ya wananchi katika kujiletea

maendeleo yao. Hivyo wizara yangu inamuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane ili tuweze kuvifanikisha na kuviletea maendeleo vijiji hivyo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kama wananchi wanapoanza na serikali huwasaidia na tayari wananchi wa kijiji cha Mwane wameshajipatia nguzo zao 9 na Kivugo Kiungoni nguzo zao 10. Ni lini zitasimamishwa nguzo zile ili zinusurike kuliwa na mchwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli wananchi hao wameshatafuta nguzo 19 ambazo wameshaziweka, lakini Shirika la Umeme tayari limeshafanya tathmini yakuvuta line kubwa katika kijiji hicho ambayo tathmini hiyo ina thamani ya kiasi cha fedha milioni 17 ambazo zitakapokamilika pesa hizo ndipo utapelekwa umeme katika kijiji hicho.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, tunakumbuka kuwa Shirika la Umeme kazi ni kutoa huduma za kusambaza umeme kwa wananchi, wananchi wa kijiji cha Gongomawe kadhalika na wao walishatayarisha nguzo, waya na kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya kuungisha umeme. Je, nini mchango wa shirika katika kuwapatia wananchi huduma hiyo muhimu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii swali hili nitalijibu kwa faida ya ukumbi hii, ni kwamba eneo hili la Gongomawe tumesikia na tutalipitia katika ziara nitakayoifanya hivi karibu Kisiwani Pemba kuangalia hayo yaliyokusanywa kwa sababu kama wananchi wamejitahidi wamekusanya nguzo, waya na vitu vyengine sioni sababu kwa nini wananchi hao wasipate umeme. Kwa hivyo, naahidi katika ziara nitakayoifanya hivi karibuni Pemba nitalipitia eneo hilo na nitashirikiana na Mhe. Mwakilishi tukaliangalie kwa pamoja halafu tutizame jinsi ya kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu serikali ina adhma ya kuwaondolea wananchi matatizo ya umeme katika vijiji vyote vilivyomo Unguja na Pemba na hilo ndilo kusudio la serikali kwa sababu kijiji hiki cha Kivugo kilichaekewa ahadi siku nyingi sana na tulipokuwa kwenye kamati Mhe. Naibu Waziri aliahidi kwa sababu wameshakusanya nguzo zao basi tatizo lao litatatuliwa mara moja, na kwa vile muda umeshakuwa mrefu.

Je, Mhe. Waziri ni lini hasa watu hao wataondolewa tatizo hili ili zile nguvu za mwakilishi aliyepita zionekane kama zinafanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ina malengo yakuwasambazia umeme wananchi wake wote wa Unguja na Pemba na jambo hili tayari limeshafanyika. Kwa hivyo, Mheshimiwa kijiji chako hicho pale hali ya fedha itakaporuhusu nacho kitamaliziwa na kitaunganishiwa umeme huo.

Nam. 51

Uchimbaji wa Kisima Shehia ya Kinyasini

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Ukosefu wa maji ni tatizo kubwa sana katika Jimbo la Chaani hasa katika maeneo ya Kinyasini na Moga. Katika Mkutano wa kampeni tarehe 13-11-2010 uliofanyika Jimbo la Mkwajuni Rais wa Zanzibar aliahidi uchimbaji wa kisima katika Shehia ya Kinyasini.

Je, uchimbaji huo utaanza lini ili kuwaondolea adha wananchi wa Kinyasini na maeneo jirani ya Jimbo la Chaani na Kitope.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kipindi cha kampeni za kuomba ridhaa za wananchi, ahadi mbali mbali zilitolewa takriban na wagombea wote wa ngazi tofauti kuanzia nafasi ya Urais, Ubunge, Uwakilishi na Udiwani.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itazifuatilia ahadi za Mhe. Rais zinazohusu matatizo ya maji ili kuzipangia taratibu za ufanikishaji.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa sekta ya maji ni sekta muhimu sana kwa maisha yetu na hivi sasa tunaelekea katika mfumo wa maji wa wananchi kulipia.

Je, serikali haioni kuna umuhimu wa sekta hii kuiweka binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza sikubaliani nae kusema kwamba serikali imeshindwa kuwasambazia wananchi maji, isipokuwa tu hayo ni matatizo ya kawaida ambayo wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inajitahidi kuyafuatilia na kuyashughulikia na itahakikisha itawapatia wananchi maji safi na salama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kijiji cha Paje muda mfupi kinategemea kupokea wageni elfu sita mpaka elfu kumi kwa shughuli ya jitimai na wamehangaika karibu miaka miwili au mmoja na nusu kutatua tatizo la maji na mpaka muda huu hawajapatiwa ufumbuzi na keshokutwa wanategemea kupokea wageni na bila ya kuwepo maji panaweza pakatokezea maradhi.

Je, Serikali imepanga vipi kulitatua tatizo hili kwa wananchi wa Paje.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, tutawasaidia kadiri itakavyowezekana pindi na wao wenyewe wakijitayarisha kutafuta vifaa kama walivyofanya wengine na mafundi wa maji tutapeleka na kuanza kufanya *survey* mapema ili kugundua mahitaji ya hiyo dharura maana hayo ni mahitaji ya dharura kwa sababu ya jitimai. Kwa hivyo, mimi nina hakika mafundi wangu na wao watapenda waitekeleze hiyo dharura ili na wao wapate thawabu za jitimai.

Mhe. Muhammed Haji Khalid: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa tatizo la maji ni tatizo kubwa la kitaifa katika jimbo langu na katika sehemu yangu mimi binafsi kampuni fulani ya maji ilichimba visima kadhaa kwa kupeleka maji Jimbo la Kiwani, hasa viko visima vitatu ambavyo vimechimbwa na havitumiki na katika jimbo langu vijiji vya Mgungu na Mahudusi kuna tatizo la maji. Je, wizara haioni haja visima hivi kuvitumia ili tukapata maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, Nishati: Mhe. Spika, kwanza kuna utaratibu maalum wa kuchimba visima kila maeneo yanapohitajika na huwa mara nyingi tunawahimiza wananchi wanapokuwa na dhamira ya kuchimba kisima waonane na wataalamu wetu kwanza kutafuta hilo eneo ambalo maji safi na salama yanaweza yakapatikana kwa sababu sio rahisi wala sio sahihi kila utakapochimba kisima utapata maji safi na salama. Mhe. Spika, sehemu nyingi watu wanachimba kisima na matokeo yake wanapata maji ya chumvi. Kwa hivyo, kama sehemu hii inayozungumzwa visima vimechimbwa na maji safi na salama yamepatikana msaada unaohitajika hapa kama haupo ni kutafuta pump ili maji yale yapigwe pump yaweze kuwafikia wananchi.

Mhe. Spika, nasema hilo nalo naliwekea ziara yangu ya Pemba na namuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane kuvikagua visima hivyo halafu baadae tunaweza kutafuta mbinu za kuwasaidia ili wananchi waweze kupata maji.

Nam. 60

Sifa za Hospitali ya Wilaya

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Tumekuwa tukifahamishwa kwamba sasa Serikali imekusudia kuzipandisha hospitali zilizopo nchini katika daraja mbali mbali zikiwa ni pamoja na ngazi ya Wilaya, Mikoa na hata Hospitali ya Mnazi mmoja kuwa ni Hospitali ya Rufaa.

(a) Je, Mhe, Waziri ili hospitali iwe na hadhi ya kuitwa ya Wilaya, inahitajika iwe na sifa gani.

(b) Je, Serikali inakusudia kuzigawa hospitali za watu binafsi (Private Hospitals) katika daraja kama hizo za Hospitali za Serikali.

(c) Kama haifikirii kuzipanga katika daraja za Wilaya na Mikoa, je ina utaratbu upi wa kuzigawa katika ngazi mbali mbali kulinganisha na sifa zao za kiutendaji na kiufanisi katika kutoa huduma, ili kuwasaidia wananchi wetu na wageni kutoka nje ya nchi kupata matibabu bora.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa ujumla kuna hospitali tatu za Wilaya hapa Zanzibar ambazo zote ziko Pemba (Chake chake, Wete na Mkoani) ili hospitali iwe na hadhi ya kuitwa Hospitali ya Wilaya inahitajika iwe na sifa zifuatazo:-

Muundo: Inatakiwa iwe na vitanda vya kulaza wagonjwa kuanzia 80 hadi 120 (Wete 110, Chake 120 na Abdalla Mzee 80).

Huduma zinazopaswa kutolewa:

(i) Iwe inatoa ushauri wa kitaalamu wa afya katika fani mbali mbali ikiwemo magonjwa ya wanawake na uzazi (*Obstetrics and gynaecology)*, huduma za upasuaji (*Surgery*), matatibabu

ya mifupa *(Orthopaedics)*, huduma za watoto na magonjwa ya macho na akili.

(ii) Iwe inatoa huduma za uchunguzi wa maradhi *(Laboratory and X-ray).*

(iii) Iwe inapokea rufaa kutoka hospitali za vijijini.

(iv) Iwe inatoa huduma za elimu ya afya na ushauri nasaha.

(v) Iwe ni sehemu ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa Chuo cha Afya.

(vi) Iwe inatoa huduma katika ngazi ya jamii kwa kufuatilia wagonjwa majumbani.

(vii) Iwe inatoa huduma za kumrejesha mgonjwa katika hali ya kawaida (*rehabilitation*) pamoja na huduma za viungo (*physiotherapy*) kazi za vitendo *(occupational therapy).*

(viii) Hospitali ya Wilaya inatakiwa pia iwe na uwezo wa kutoa huduma vijijini (*Outreach services*) na kufanya tafiti *(Operational research).*

Chanzo: Maelezo haya ni kwa mujibu wa kitita cha utoaji wa huduma muhimu za afya za msingi *(Essential Health Care Package Primary Level pamoja na Health Sector Reform Strategic Plan II).*

(b) Kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kuzigawa hospitali binafsi kama ilivyo kwa muundo wa hospitali za Serikali. Mgawanyo wa hospitali binafsi uliopo hivi sasa ni:-

(i) Hospitali za Mijini.

(ii) Hospitali za Vijijini.

Nazo zimegawanyika katika:-

(i) Hospitali za kulaza wagonjwa (Al Rahma, Marie Stopes na ZMG)

(ii) Zahanati (dispensaries) hizi zipo 78, 68 Unguja na 10 Pemba.

Mhe. Mbarouk Haji Wadi (Mtando): Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuwa kwenye kampeni za uchaguzi kwenye mkutano wake wa hadhara wa Kibeni aliahidi kwamba hospitali ya Kivunge itakuwa hospitali yenye hadhi ya Wilaya. Je, ni lini hospitali hii itakuwa tayari kuwa na hadhi ya Wilaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Rais alipokuwa katika ahadi za kampeni alisema kwamba hospitali ya Kivunge na hospitali nyenginezo ambazo zilikuwa cottage zitafanywa kuwa hospitali za Wilaya. Mhe. Spika, ni kwamba maandalizi ya hospitali hizo ni kama yale niliyosema mwanzo kwamba tangu tuiingie madarakani nafikiri ni miezi mitatu tu. Kwa hiyo kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba yale yote niliyoya-list yamekamilika na Mhe. Rais atatawala kwa miaka mitano. Kwa hivyo, nakuhakikishia kuwa kipindi cha miaka mitano wakati wowote hospitali hiyo itakuwa ni hospitali ya Wilaya.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mhe. Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nikiupongeza mpango mzima wa serikali wa kuzipa hadhi zaidi hospitali zetu kwa maana ya kutoa matibabu bora.

Mhe. Spika, ni kwamba lakini hadi leo kuna sehemu ambazo watu wake wanapata shinda sana ya matibabu kiasi ambacho wamejijengea vituo vya afya kwa kutumia nguvu zao wenyewe, na wameomba msaada katika serikali bado haujafanikiwa, sijui Mhe. Waziri atanipa maelezo gani kuhusu kituo cha Bwagamoyo kilichopo katika Shehia ya Piki Mtambwe ambapo wananchi kwa dhiki ya huduma wanayoipata ya afya wamejitahidi kujenga kituo mpaka sasa hivi tayari wameshaezeka na kutia madirisha kwa kumalizia sehemu iliyobakia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakumbuka hapa nyuma tulizungumza wakati Mhe. Waziri wangu alipokuwa anatoa taarifa ya Wizara ya Afya alisema kwamba Zanzibar imefikia asilimia 95 ya wananchi wanaokwenda hospitali chini ya kilimita 5 na hilo ndio lengo la utaratibu kwamba nchi yoyote iliyokuwa na utaratibu wa kutawanya vituo vya afya ili wananchi waweze kufika katika sehemu ya kituo cha afya, isipungue wala isizidi kilomita 5. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Zanzibar kuliko nchi nyengine nyingi duniani imefikia hilo lengo, kwa hiyo hali yetu ni nzuri. Kwa hivyo, kwanza ni kuhakikisha kwamba tunaviimarisha vile vituo hakuna wafanyakazi, hakuna madawa hivyo tuviimarishe vituo ili viweze kutoa huduma. Lakini pale pindipo wananchi wameshafanya hivyo basi tuna haki kama serikali kuwaunga mkono kumaliza hivyo vituo.

Mhe. Spika, mimi naomba niwashauri Waheshimiwa Wawakilishi kwa hisani zetu sasa hivi msihakikishe mnaendelea kujenga vituo kwani itatuwia vigumu kuweza kuvikidhi haja hivyo vituo kwanza acha bora tuifanye hii kazi ya kusambaza wafanyakazi, tusambaze huduma ndio baadae tuone kama kuna haja ya kuongeza vituo tushauriane tupite katika wizara ili tukubaliane ndipo mjenge hivyo vituo.

Mhe. Spika: Kuna jambo alilitaja Mheshimiwa kuhusu kituo chake cha Mtambwe ndio hilo jibu alililokuwa analitaka.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mhe. Spika, kwa kumsaidia Mhe. Waziri ni kuwa hiki kituo kilijengwa kwa ushauri na Wizara ya Afya na wizara hii ndio iliyoshughulikia kikamilifu katika kutoa plan na kuomba misaada na kuleta mafundi. Sisi ikawa tunatumia jasho na msaada tulionao mpaka tukafika hapo kwa mashirikiano hatukujenga tu kwa utashi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ninachokumbuka mimi na yeye tulishazungumza suala lake hili na nilimuahidi kwamba tutajitahidi kama tunavyoweza twende tukatembelee na tuone kile kinachohitajika kukamilisha. Kwa hivyo, naendelea kumuahidi kwamba tutakwenda tuone kinachohitajika ili tukamilishe. Nashukuru kwa hilo.

Nam. 44

Wanafunzi Kupatiwa Vikalio

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba watoto wote wanaofikia muda wa kuanza masomo ya msingi wanapatiwa nafasi katika skuli mbali mbali za Serikali nchini, bado tunakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa vikalio vya kutosha kwa wanafunzi wetu.

(a) Je, Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inalishughulikia tatizo hilo kwa haraka na bila ya kungoja misaada ya wafadhili.

(b) Je, wizara imeandaa mpango gani endelevu wa kumpatia kikalio kila mwanafunzi anayehudhuria skuli.

(c) Kwa kuwa hadi hii leo bado tunakabiliwa na tatizo hilo. Je, wizara inatuahidi mwaka gani itahakikisha kwamba imefikia lengo la kumpatia kila mwanafunzi kikalio chake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.44 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli skuli zetu zinakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa vikalio kulingana na ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi.

(a) Mhe. Spika, wizara imelipa uzito mkubwa suala hilo na kwa mwaka wa fedha 2009/2010 wizara ilitenga jumla ya shs. milioni 120 kwa ajili ya kuchongesha vikalio na yalipatikana madeski 700 kwa skuli za Unguja na madeski 500 kwa Pemba. Pia, kwa mwaka 2010/2011, wizara yangu imetenga jumla ya Shs, milioni 250 kwa ajili ya uchongaji wa madeski 1,250 ambayo yatasaidia kupunguza uhaba huo.

(b) Wizara inaandaa mradi mkubwa kwa ajili ya uchongaji wa vikalio vya maskuli na baadae kumtafuta mhisani ambae atatusaidia. Aidha, pia inatoa mafunzo kwa walimu juu ya njia ya utunzaji na matengenezo ya vikalio viliopo maskulini.

(c) Kwa hivi sasa ni mapema sana kujua lini tatizo la vikalio maskuli litamalizika. Hata hivyo, ni azma ya wizara yangu kuhakikisha kuwa tatizo la vikalio maskulini linamalizika katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu wa Saba.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri yakutia moyo ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu iliwahi kupata mfadhili anayeita OPEC ambalo ni shirika lenye kukusanya nchi nyingi zinazozalisha mafuta duniani. Ni sababu zipi zilizofanya kwamba asiendewe tena mfadhili huyu na tatizo letu limeongezeka.

b) Itakapofika Januari, 2014 tutakuwa tumetimiza miaka 4 ya Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa lakini pia tutakuwa tunatimiza miaka 50 nusu karne ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea mapinduzi. Mhe. Waziri haoni haja ya kuitangaza siku hii kwamba ndio mwisho wa tatizo la vikalio vya wanafunzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nimesema kwamba tutawatafuta wafadhili kwa hivyo ni pamoja na huyo OPEC na wengineo wengi kwa hiyo atakayejichomoza kutusaidia tutampokea hatuna tatizo kwa sababu shida tunayo ya vikalio mashuleni.

Juu ya suala la kusema kwamba mwaka 2014 iwe tunamaliza tatizo la vikalio nasema ni rai nzuri lakini sitoitangaza hapa ikabidi tukaifanyie kazi kuona resources zitakazoweza kupatikana na kumaliza suala hili maana suala lenyewe sio dogo. Mhe. Spika, kuna madarasa ambayo yameshamalizika, kuna madarasa hayajamalizika na ni mengi kweli, kuna skuli karibu 60 zina madarasa ambayo hayajamalizika na yote yanahitaji vikalio. Kwa hivyo, lazima tufanye hesabu vizuri ili commitment tutakapoitoa iwe na maana sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, hili tatizo la vikalio likimalizika kwa Zanzibar nzima ni nini mahitaji yote kwa jumla ni idadi gani inahitajika ipatikane ili tatizo hilo limalizike kwa Zanzibar nzima.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anauliza figer ambayo ni kubwa sana kutokana na ongezeko la wanafunzi kama tunataka kila mwanafunzi akae kwenye vikalio basi tutizame kama darasa moja linakuwa na watoto 130, tukazihisabu skuli zetu kwa kweli ni idadi kubwa sana lakini kama anataka nimfanyie nimletee nitamletea kabisa aone ule ukubwa wake.

Lakini hata hivyo nataka nitumie nafasi hii kidogo kutoa wito. Mhe. Spika, huu mzigo ni mkubwa sana mimi naomba kwamba tutakapokuwa tunapitisha zile fedha za maendeleo katika majimbo nafikiri waheshimiwa waliomo humu ndani waeke mkazo kwa vikalio katika maskuli yao zaidi pamoja na wabunge waeke mkazo vikalio katika maskuli yao kwani itasaidia serikali kupunguza suala hili. Mhe. Spika, kuna mifano ya wabunge wameshaanza kutoa vikalio katika maskuli yao na wanasaidia kulipunguza hili tatizo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na matatizo ya vikalio lakini pia pana wimbi kubwa la upungufu wa walimu, na walimu wengi sasa hivi wameshasomea wako nje si chini ya miaka mitatu. Je, tatizo hili litamalizika lini.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, tatizo la upungufu wa walimu unaweza ukasema lipo kwa sababu tuna upungufu wa walimu wa sayansi, lakini kwa kuwa na walimu tunashukuru Mwenyezi Mungu katujaalia tuna walimu wengi sana na katika baadhi ya Mikoa walimu wamefurika hasa. Kwa mfano, hapa Mkoa wa Mjini skuli za msingi peke yake kuna walimu 780 wamezidi na wapo katika maskuli mbali mbali. Sasa hivi mkazo tunaoweka ni kuhakikisha kwamba tunapata walimu kwa mujibu wa mahitaji yetu wa kusomesha sayansi, hesabu na mambo mengineyo lakini tunao

wengi. Na hao walimu walioko nje kidogo kidogo tutakuwa tunawameza wawe wana subra tu.

Nam. 69

Kushamiri kwa Vitendo vya Unyanyasaji wa Kijinsia

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) – Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu unyanyasaji wa kijinsia unaofanywa dhidi ya akina mama na watoto, ikiwa ni pamoja ubakaji na utelekezaji wa watoto.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kukomesha vitendo hivyo.

(b) Je, ni kesi ngapi wizara imesimamia kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Ni washtakiwa wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria na wangapi wameachiwa huru.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuliona tatizo hili limekithiri na kuhatarisha maisha ya wananchi wake imeweza kulivalia njuga na kulitafutia ufumbuzi muafaka.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a) na (b)kama ifuatavyo:-

b) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuliona tatizo hili limekithiri na kuhatarisha maisha ya wananchi wake imeweza kulivalia njuga na kulitafutia ufumbuzi muafaka. Miongoni mwa jitihada zilizofanywa ni pamoja na:

Kuanzishwa Kamati ya Kitaifa ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji inayowajumuisha watendaji kutoka Sekta ya Polisi,

Mahkama, Mkurugenzi Mashtaka, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, NGOs na Washirika wa Maendeleo. Mwenyekiti wa Kamati hiyo ni Kamishna wa Polisi Zanzibar. Kamati hiyo ina jukumu la kuharakisha harakati za kupunguza vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji Zanzibar.

Kumeundwa kamati za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia za Mikoa, Wilaya na Shehia Unguja na Pemba.

1. Kumeanzishwa madawati ya kijinsia katika vituo vya Polisi

2. Kumeandaliwa Mswada wa Sheria ya mtoto ambayo itakapokamilika itasaidia kuondosha tatizo hili kwa kiasi kikubwa kwa upande wa watoto.

3. Zanzibar kuanzisha kituo rafiki *(One Stop Centre)* cha Majaribio kwa Unguja na Pemba.

4. Kituo cha huduma rafiki *(One Stop Centre)* ni kituo ambacho kinajumuisha huduma zote zinazohusiana na ushughulikiaji wa matukio unyanyasaji wa kijinsia, kituo kinajumuisha wahudumu wa afya. Polisi, Wanasheria na watoa ushauri nasaha kwa wahanga wa unyanyaswaji na udhalilishaji. Kituo hicho kipo Mnazimmoja Hospitali na kwa upande wa Pemba hatua za uanzishaji zinaendelea katika Hospitali ya Chake Chake.

Mhe. Spika, naomba kumjibu kuwa kutokana na mipaka ya kitaasisi, wizara yangu haina mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa kesi za utelekezaji wa Wanawake na watoto bali hutoa ushauri nasaha kwa wale waliofikwa na tatizo hilo na wameripoti Wizarani.

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto imepokea malalamiko mbali mbali ya Wanawake na watoto. Kwa mwaka 2007/2008, Idara imepokea jumla ya malalamiko 429, (Unguja 234 na Pemba 195). mwaka 2008/2009 Idara imepokea jumla ya malalamko 384 (Unguja 157 na Pemba 227) mwaka 2009/2010 Idara imepokea juma ya malalamiko 506 (Unguja 314 na Pemba 192) ikiwa ni pamoja na malalamiko ya kubakwa,

mimba za utotoni; kutoroshwa, mvutano wa malezi, kufukuzwa nyumbani na kudhalilishwa.

Malalamiko ya Watoto yaliyoripotiwa katika Idara ya Ustawi wa Jamii tokea Februari 2009 hadi sasa ni 257. kwa upande wa Unguja malalamiko yaliyoripotiwa ni 168. Kesi za kubakwa ni 41 ambapo 10 zipo Mahkamani 31 zipo katika uchunguzi wa Polisi, kutelekezwa malalamiko 111, ambapo malalamiko 100 yamepatiwa ufumbuzi, wazazi wameitwa na wamekubaliana kusaidiana katika malezi, 11 zinashughulikiwa na kesi za kulawitiwa ni 5 ambapo 3 zipo mahakamani na 2 ziko polisi.

Kwa upande wa Pemba jumla ya malalamiko ya watoto yaliyoripotiwa ni 89 ambapo malalamiko ya kubakwa ni 37 na yote yapo mahakamani, malalamiko 43 ya kutekelezwa ambapo wazee wa watoto hao wameshaitwa na yameshapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, kuhusu kufahamu kesi ngapi za Watoto na Wanawake ambazo zimepelekwa mahakamani na ngapi zimeshatolewa hukumu, kwa sasa ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP) ndio wanaopeleleza na kushtaki kesi zote zinazohusu jinai, hawana mfumo wa kuweka kumbukumbu na mchanganuo wa kesi zinazohusu wanawake na watoto. Aidha, hakuna mfumo wa utuatiliaji kesi *(Case Tracing System)* ambao ungeweza kupatikana kwa taarifa ya kufahamu kesi ipo katika hatua gani.

Aidha, wizara yangu imejipanga kufuatilia suala hili ili iweze kufahamu jumla ya kesi zote zinazohusu wanawake na watoto ambao zimefikishwa mahakamani zipo katika hatua gani. Mhe. Spika, pia Wizara yangu imepanga kukaa pamoja na ofisi ya Mwendesha Mashtaka ili kuweka sawa suala hili na kuweza kulipatia ufumbuzi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza sula moja la nyongeza.

Kwa kuwa kesi za unyanyaswaji zinazidi kila siku katika kisiwa cha Pemba pamoja na vijiji vya Unguja. Je, Wizara yako imejipanga vipi kwa kuahakikisha kwamba kesi hizi zinapungua.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Kwanza napenda niwajulishe kwamba suala hili la uzalilishaji wa watoto pamoja na wanawake si suala la serikali tu, hili ni suala letu sote kwa ujumla wananchi, inaonekana dhahiri kwamba sasa hivi upo mmong'onyoko

mkubwa wa maadili katika nchi yetu. Tunaambiwa laatakrabu dhina usiikaribie dhina lakini ndio kwanza watu wanashadidia katika mambo haya.

Kwa hivyo, naomba wananchi tujipange sisi kushughulikia mambo kama haya vyenginevyo tutafika katika hatua mbaya sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala la nyongeza.

Mhe. Waziri hivi karibuni tulisikia katika Redio ya Zenj FM kuna dereva mmoja wa Mkoa wa Kaskazini amembaka mwanamke na kumtia mamba. Je, Mhe. Waziri Wizara yako inayo habari, na kama ina habari mpaka sasa hivi umechukua hatua gani.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Na mimi suala hilo nililisikia ndani ya redio na nimefuatilia nikakuta mambo mawili ambayo yanatuhumiwa.

1) Moja ni kufanya tendo hili kwa njia ya kawaida ambayo watu wanaitumia na kuifanya.

2) Ni kufanya kinyume cha maumbile ambacho hakiruhusiwi kabisa, kinaweza kuruhusiwa ikiwa mnaweza kukubaliana nyinyi wenyewe. (*Kicheko*).

Kwa sababu aliyefanya tendo hili ni dereva wa Mhe. Mkuu wa Mkoa nadhani kwanza Mkuu wa Mkoa atatusaidia akiwa huyu ni mfayakazi wake wa karibu. Lakini hata mimi nilipata nafasi ya kuzungumza na huyu dereva na nikamuasa kwamba tendo hili sio tendo zuri.

Mhe. Spika, lakini nilikuwa najiuliza nani hawa wanaofanyiwa vitendo viovu siku zote ni wanawake au watoto, wanaofanya ni nani wanaume ndio wanaofanya. Kwa sababu hapa kuna waheshimiwa wawakilishi kutoka kwenye majimbo, kutoka viti maalum naomba tunapokwenda kwa wananchi wetu basi tuwaelimishe juu ya haya, sisi tumechukua hatua mbali mbali kama vile makongamano tunayafanya, kuna semina tunazifanya katika shehia zetu, katika vijiji vyetu, katika mikoa yetu. Lakini naomba na nyinyu musaidie jambo hili jamani tuliacheni tena basi.

Mhe. Spika: Namwambia Mhe. Waziri kwa sheria zetu ile kauli ya kwanza ndio sahihi hairuhusiwi kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Viwe Abdalla Khamis: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kuhusu watoto wa mitaani ambao wametekelezwa na watoto wao je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwasaidia ili waondokane na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Ni kweli watoto wa mitaani wapo wanaomba omba wanadhurura, na wengine wametelekezwa na wazazi wao, serikali itajitahidi wakati wowote hali yetu itakaporidhisha basi serikali itajitahidi kusaidia kuondoa wingi wa watoto hao wa mitaani ili tuwarudishe katika makazi yao.

Nam. 17

Utembezaji wa Wageni

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Alijibu:-

Kwa kuwa baadhi ya wamiliki wa Hoteli za Kitalii hufanyakazi za kuwatembeza watalii katika maeneo mbali mbali; na kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume na utaratibu wa kazi zao; na kwa kuwa jambo hili limekuwa linalalamikiwa sana na watembezaji watalii *(Tour Guider*).

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuendelea kuwaachia wamiliki mahoteli kutembeza watalii kunawanyima ajira vijana wetu wazalendo ambao tayari wameshasajiliwa na Serikali kwa kazi hiyo.

(b) Je, Serikali itachukuwa hatua zipi ili kuondosha jambo hili.

Mhe. Naibu Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba baadhi ya wamiliki wa Hoteli za Kitalii hufanya kazi za kutembeza watalii kadhia hiyo ilikuwepo hapo nyuma na suali hili limezungumzwa katika kikao cha Pili cha Baraza la Biashara Zanzibar *(Zanzibar Business Council)* katika kulifanyia kazi suala hili Kamisheni ya Utalii, Jumuiya ya Watembezaji Watalii (ZATO) na Jumuiya ya Wawekezaji wa Utalii (ZATI) walifanya vikao

vine ambapo ilikubaliwa kwamba wamiliki wa hoteli wasite mara moja kufanya kazi hii ikiwa pamoja na transfer.

(b) Mhe. Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kuondoa kadhia hii ni kama zifuatazo:-

i) Kufanya vikao vya pamoja na wamiliki wa mahoteli kulizungumzia kwa kina suali hili na athari yake kwa wazalendo.

ii) Kuwapa onyo na kuwapa adhabu (*fine*) wamiliki wa mahoteli ambao waliofanya kazi hii.

iii) Kuweka katazo hilo katika leseni zote za hoteli za kitalii.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba suala hilo mpaka sasa hivi kwenye mahoteli linatendeka. Kama ni hivyo serikali inachukua jitihada gani ili kulimaliza kabisa kama tunavyosema kwamba tuna serikali ya kitaifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwakilishi nakubaliana na wewe lakini kwa sababu maelezo yote nimeeleza humu suali hili liko na limeshafuatiliwa na Wizara pamoja na Serikali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja.

Kwanza nilikuwa naomba Mhe. Naibu Waziri aendelee kutuelimisha ni hatua zipi ambazo serikali imechukua ili kukomesha suala hili kwa sababu kama ilivyoelezwa hapa linaendelea, hivi karibuni tu mimi katika ziara zangu katika Jimbo la Mji Mkongwe imeonekana hoteli nyngi za kitalii bado zinajishughulisha na suala hili.

1) Moja serikali inachukua hatua zipi ili kulikomesha suala hili mbali ya hizo hatua alizokwisha kuchukua.

2) Pili inaonekana katika wanaofanya shughuli hizi mbali ya kwamba ni wenye mahoteli lakini pia sheria inakataza kufanywa na wasiokuwa Wazanzibari, wako baadhi ya watu wanaofanya shughuli hizi sio Wazanzibari na kwa kujiingiza katika ajira hizi wanawakosesha ajira hizi vijana wa kizanzibari. Je, pia wizara inachukua hatua gani ili kukomesha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, hili suala lipo na wizara inayo taarifa hiyo lakini Wizara yangu imekusudia kuanza kufanya ziara kwa mahoteli yote na vile vile kuipitia mikataba yote, tumekusudia kwamba kama kitendo hichi kitakuwa kinafanyika basi tuna uwezo hata wa kumzuilia leseni lakini kwa kushirikiana na Wizara husika inayohusiana na mambo ya investment kwa sababu hatuko peke yetu. Kwa hivyo tutashirikiana na kutizama uwezekano hata wa mtu kumnyima leseni.

Nam. 56

Uwekaji wa Eneo Maalum la Uvuvi

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa – Aliuliza:-

Eneo la Mangapwani linasadikiwa kuwa maarufu kwa mazalio ya samaki; lakini mazingira yake yamo hatarini kutokana na kufunga nanga meli zenye uzito mkubwa.

(a) Kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira ya bahari yetu Serikali ina mpango gani kukabiliana na tatizo hilo.

(b) Kwa kuwa eneo hilo lipo hatarini Serikali imeweka eneo jengine kwa wavuvi wa eneo hilo ili kuzuia uharibifu wowote unaoweza kutokea kama zinavyofanya nchi nyengine duniani.

(c) Kwa kuwa wavuvi wetu vifaa vyao vya kuvulia ni vyepesi, Serikali imeandaa mpango gani wa kukabiliana na mtu yeyote anayehujumu vifaa hivyo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Kabla sijamkera naomba nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa kuonekana kukerwa na majaribio ya uharibifu wa mazingira ya bahari yetu. Naomba nichukue fursa hii kumuomba kila mjumbe wa Baraza lako tukufu na kila kiongozi na kila mwananchi wa Zanzibar kuiga mfano wa Mhe. Mwakilishi katika kukerwa na uharibifu wa mazingira ya bahari yetu na kujitolea kuchukua kila hatua za kurekebisha athari za uharibifu huo.

Aidha, naomba nitoe maelezo kwamba mara nyingi meli zenye uzito mkubwa hutia nanga kwenye maji ya kina kikubwa ambayo kwa kawaida huwa hayana matumbawe au sehemu ambazo samaki huzaliana.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi.

a) Ili kuepusha uharibifu wa kimazingira unaoweza kusababishwa na ufungaji wa nanga, Wizara yangu imekuwa ikiweka maboya maalum ya kuegeshea vyombo (mooring buoys). Hata hivyo, maboya hayo ni kwa ajili ya boti za uvuvi za kienyeji na za kiutalii zinazotembelea maeneo yetu. Aidha, kwa meli kubwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ndio inayohusika na kuweka maboya hayo.

b) Mpaka wakati huu, Wizara yangu bado haijawa na tatizo kubwa na wala kupata malalamiko yoyote kutoka kwa wavuvi wetu kuhusiana na eneo hilo la Mangapwani na matumizi yake lakini Wizara yangu imelichukulia suala hilo kama ni taarifa na itaendelea kufanya utafiti wa kina kuhusu suala hili.

c) Wizara yangu inatoa elimu kwa wavuvi kuhusiana na maeneo yao ya kuvulia, inawataka wavuvi kuweka viashiria kama vile taa katika mitego yao na pia kuepuka kutega katika njia za meli. Aidha, Wizara yangu inasimamia kuhakikisha meli zinazobainika kuhujumu zana za wavuvi zinalipa fidia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, suala la hifadhi ya mazingira ni suala la kitaifa lakini kisiwani Kojani hapa ninapozungumza kuna mgogoro wa jambo hilo. Kwa sababu takriban Wakojani wote ni wavuvi na kisiwani kule kuna eneo dogo na sehemu ya bahari ndio maana muda mkubwa wanatoka kwenda dago kwamba eneo lile halitoshi. Sasa kumezuka mgogoro mkubwa kuhusiana na hifadhi ya mazingira ambayo inakwenda zake. Je. Mhe. Waziri atatatua vipi mgogoro huu kisiwani Kojani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli wananchi wa Kisiwa cha Kojani ni wavuvi wa asili tena mahiri sana. Nakubali kwamba wana mgogoro mdogo unaohusiana na masuala ya hifadhi ya bahari yao. Nimewasiliana na Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Wete leo hii asubuhi ili mimi, yeye Mkuu wa Wilaya pamoja na Mhe. Mwakilishi mara baada ya Baraza lako tukufu twende katika Kisiwa cha Kojani tukazungumze na wananchi ili suala hili la mgogoro limalizike.

Mhe. Farida Amour Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mwishoni mwa mwezi wa Disemba mwaka jana kuna meli ilihujumu wavuvi waliokuwa wakivua katika kisiwa cha Pemba na Tanga na kusababisha uharibifu mkubwa hadi hii leo mvuvi mmoja hajaonekana.

a) Je, Mhe. Waziri tokeo hilo analijua.

b) Ni meli gani hiyo iliyofanya hujuma hiyo na imechukuliwa hatua gani.

c) Ili kuepusha hujuma hiyo wizara yake imejiwekea mikakati gani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika,

(a) Suala hili nalijua ni kweli kwamba mwishoni mwa mwezi wa Disemba wizara yangu ilipokea taarifa hiyo kwamba kuna meli imewahujumu wavuvi baina ya kisiwa cha Pemba na Tanga. Mimi pamoja na ujumbe mzito wa Idara ya Uvuvi tulikwenda katika eneo la tukio, pia kuonana na familia ya mvuvi ambaye mpaka leo hajaonekana.

Mhe. Spika, kupitia Baraza hili tukufu naomba niipe pole familia ile na niwaombe waendelee kuwa na subira Mwenyezi Mungu atabainisha ama yuko hai au amefariki.

(b) Meli iliyosababisha uharibifu huo haijajulikana bado. Wizara yangu imejaribu kufuatilia suala hili na imewasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kujua ni meli ya aina gani, ilikuwa ikitokea wapi. Tukajaribu kuhangaika tukawasiliana na wenzetu walioko Dar es Salaam lakini bahati mbaya kwa siku ile iliyotokea tokeo kukawa hakuna taarifa yoyote ambayo imeeleza kwamba kuna meli ilipita ikasababisha uharibifu huo. Kwa hivyo, mpaka leo haijulikani na hakuna fidia iliyolipwa mpaka sasa.

Mhe. Spika, katika kujaribu kulitatua tatizo hilo kwa sababu taarifa kama hizi huwa tunazipata mara kwa mara. Nilipokuwa kwenye ziara yangu ya kutembelea Pemba hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambako ndiko mara

nyingi suala hili hutokea kwa sababu ya mpaka baina ya Tanzania na Kenya, nilichukua hatua nne zifuatazo.

1. Niliomba na kufanikiwa kuzungumza na kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, tumepanga mikakati mizuri ya kufuatilia jambo hilo na tutaliratibu.

2. Niliporudi Unguja nilimuandikia barua Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu, ili kuona ni namna gani Kikosi chetu cha KMKM tunaweza kufanya doria ya pamoja katika suala hili. Kikao hiki tayari tumeshakifanya. Tumeunda kamati ya wizara tatu. Wizara ya Nchi (AR) Ikulu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Miundombinu na Uchukuzi.

3. Nimemuandikia barua Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ili tukae pamoja tuone namna gani tunaweza kutumia Jeshi la Ulinzi na hasa kikosi chake cha Nevi kushirikiana katika ulinzi wa doria baharini.

Na hatua ya mwisho ya nne niliyoichukua ni:

4. Wizara yangu imetangaza zabuni ya kununua kifaa kinachoitwa Vessel Monitor Devices, ambacho kinaweza kuratibu na kujua meli ambazo zimeingia katika maeneo yetu, ili linapotokea jambo basi iwe ni rahisi kujua ni aina gani au chombo gani kilichofanya hujuma hiyo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umemalizika, lakini kwa hoja iliopo mbele yetu leo nadhani tunamudu kuimaliza na muda wa kutosha tunao. Kwa maana hiyo ningeomba sana na kwa kuwa maswali bado tunayo mengi, tungetenga kanuni yetu kando ile ya 43 ili tuweze kuongeza muda kidogo tuyamalize maswali haya, halafu twende kwenye hoja ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba tuweke kanuni kando ya maswali na majibu ili tuweze kumaliza maswali yalioko ndani ya order paper ya leo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nawashukuruni Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake za ufuatiliaji hasa kwa matukio yanayowagusa wananchi. Swali langu liko hapa.

Mhe. Spika, kwa tunavyofahamu kwamba meli zote za nje zinazopita katika bahari yetu, zina utaratibu wa kulipishwa ada ya minara ya kuongozea meli. Sasa Mhe. Waziri anasema katika kufuatilia meli hii mpaka sasa hivi hawajaijua ni meli gani na ilikuwa inatokea wapi.

Kwa hivyo, nataka kumuuliza Mhe. Waziri je, amejaribu kufuatilia katika haya mashirika yetu mawili ya bandari ambao wao ndio wanaopaswa kujua meli zinazopita na ambazo zinapaswa kulipa hizi ada za minara?

Kama hawajui taarifa hizo je, hatuoni kwamba mashirika yetu haya ya meli za Zanzibar na lile la Tanzania Bara kwamba hizi meli zinatuibia ada za minara yetu? Kwa sababu kama ingekuwa kumbukumbu hizo zipo, basi nadhani hiyo meli ingekuwa inajulikana wapi ilipotoka, kwa sababu tayari kuna ada ambazo ilipaswa kulipa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Spika. Ni kweli kwamba shughuli za usafiri wa meli baharini huwa zina utaratibu maalum. Lilipotokea suala hili wizara yangu, kama amesikia vizuri, tuliwasiliana na Afisi ya Mrajisi wa Meli ambaye kimsingi ndiye anayeratibu shughuli za usafiri wa baharini katika nchi yetu na yeye alifanya jitihada kubwa ya kuwasiliana na uongozaji wa meli katika minara, lakini bado taarifa ikawa haijapatikana hadi leo.

Mhe. Spika, naomba nilikumbushe Baraza lako tukufu kwamba kipindi hiki katika bahari yetu ya Hindi, kuna tatizo kubwa la piracy, na kwa kweli linatishia mambo mengi hasa yanayohusiana na usafiri wa baharini. Hizi meli ambazo zina utaratibu huu wa uharamia Mhe. Spika, wakati wa kukimbia hayo masuala ya uhalifu baharini, huwa zinatembea hata bila ya taa. Sasa katika kukurupuka huko Mhe. Spika, sio rahisi wakati mwengine masuala haya kurekodiwa katika masuala ya navigations ya nchi yetu. Ndio maana katika suala hilo ili kuhakikisha kwamba tunaliratibu vizuri, tukaamua basi wizara yangu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Nchi

Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tukae ili kudhibiti masuala hayo kwa pamoja.

Nam. 49

Upandaji wa Bei ya Umeme Viwandani

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kuomba kujibiwa swali langu nambari 49, naomba nisahihishe kidogo kufanya nyongeza. Katika sehemu ya mwisho ya swali iliandikwa hivi,

> "kuvipunguzia bei ya umeme ikiwa ni kama package maalum" ikamalizikia na full stop pale. Kwa hivyo, iendelee pale pale na maneno haya. "ili kutoa motisha kwa maendeleo ya viwanda".

Naomba sasa swali langu nambari 49 lijibiwe.

Inafahamika kwamba matumizi ya umeme katika viwanda ni makubwa sana ukilinganisha na matumizi hayo katika maeneo mengine. Hata hivyo, tatizo hili pia huwaathiri wafanyabiashara na kuwafanya washindwe kulipia gharama hizo kwa ukamilifu.

Je, kwa njia gani tunaweza kuvisaidia viwanda vyetu nchini kwa kuvipunguzia bei ya umeme ikiwa ni kama 'package' maalum.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli gharama za matumizi ya umeme katika sekta ya viwanda ni kubwa kulinganisha na matumizi ya maeneo mengineyo.
Mhe. Spika, ni kweli vile vile kwamba gharama za matumizi ya umeme zimekuwa zikipanda siku hadi siku kutokana na hali halisi.

Mhe. Spika, wizara inatambua kuwa serikali ina mradi mkubwa wa kuimarisha uingizaji wa masuala ya umeme pamoja na usambazaji hapa nchini. Ni imani ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwamba mradi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za uzalishaji katika sekta ya viwanda.

Endapo hata baada ya mradi huo Mhe. Spika, kukamilika bado gharama zitakuwa kubwa, basi serikali kupitia wizara husika, hazitosita kuangalia uwezekano wa kuweka utaratibu au mfumo utakaosaidia, kwani ni azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuleta Mapinduzi ya Viwanda hapa nchini.

Nam. 59

Meli Kugawana Mafuta Kinyume na Utaratibu

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Aliuliza:-

Imebainika kuwa zipo baadhi ya meli zinazobeba mafuta hutia nanga nje ya Bandari ya Zanzibar karibu na maeneo ya Mangapwani. Meli hizo zinakisiwa kubeba mafuta ya aina mbali mbali kiasi ya tani 100,000 na kuyagawa mafuta hayo kwa meli nyengine za kubebea mafuta zenye wastani wa tani 50,000.

(a) Je, Mhe. Waziri Serikali inapata pato lolote kwenye shughuli hiyo ya kugawana mafuta.

(b) Kwa kuwa zoezi la kugawana mafuta linaweza kuleta athari kwa fukwe zetu, Je, Mhe. Waziri, pato linalotozwa wahusika linafidia athari hizo.

(c) Ni meli ngapi ambazo zimekamatwa kuhusiana na shughuli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Zanzibar kijiografia imekaa katika eneo muafaka ambapo bahari yake inakuwa shuari kwa kipindi karibu cha mwaka mzima. Sababu hiyo imepelekea shughuli za uhaulishaji wa mafuta kufanyika Zanzibar katika maeneo ya Mangapwani, badala ya kufanyika Mombasa au Dar es Salaam.

Kazi hiyo ya uhaulishaji wa mafuta ni biashara inayoendeshwa kihalali, kwani kibali cha kuingiza meli nchini kinatolewa na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na ruhusa ya kushusha mafuta toka melini kwenda nyengine hutolewa na wizara yangu.

Aidha, kazi hiyo husimamiwa kwa karibu na Maafisa wa Kikosi cha KMKM, Maafisa wa TRA na Shirika la Meli ambalo ndio shirika linalohusiana na masuala ya uwakala wa meli za kigeni.

Wizara yangu imeteuwa Kampuni ya Sturrook – Flez Shipping Ltd ya Uingereza, yenye makao yake mjini Dar es Salaam kusimamia kuzifunga meli hizo kwa ajili ya kulinda uchafuzi wa mazingira katika bahari yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inapata pato lake kama ifuatavyo: Mamlaka ya kusimamia usafiri wa baharini hupata mapato kwa kutoa kibali cha kufanyanyia biashara hiyo; Shirika la Meli hupata mapato kutokana na Uwakala wa Meli hizo na TRA hupata mapato kutokana na ukusanyaji wa kodi ya biashara husika.

(b) Kama nilivyoeleza hapo juu kuwa wizara yangu imeajiri Kampuni ya Sturrook – Flez Shipping Ltd ya Uingereza, ambayo ndio yenye utaalamu wa hali ya juu kuhusiana na shughuli hiyo. Aidha, mafuta yanayoshushwa na kupakiwa ni mafuta yaliyosafishwa, hivyo hayana athari kubwa kwa fukwe zetu. Hata hivyo, ikitokea kumwagika mafuta hayo ya kuendesha mitambo ya meli, kuna utaratibu wa kimataifa wa kimataifa wa kulipa fidia ya athari za kimazingira ambapo meli zote za mafuta hutakiwa kuwa na bima maalum, kwa maana ya kwamba kinga ya mazingira kwa ajili ya fidia pindi janga likitokezea.

(c) Hakuna meli yoyote iliyokamatwa, kwani kama nilivyoeleza awali kuwa biashara hii inaendeshwa kihalali, sio biashara ya magendo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyengine tena. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atuelekeze ni vyombo vya aina gani vinavyotumika katika harakati za kuyahaulisha mafuta hayo kutoka melini hadi kuja kwetu huku kwa ajili ya matumizi, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu mama nimesema kuna Kampuni ambayo tumeiteuwa, kampuni hii huzikutanisha meli mbili, wao wenye kampuni ndio wenye vifaa vinavyohusiana na uhaulishaji wa mafuta hayo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, na mimi vile vile nataka kujua.

(a) Baadhi ya mafuta huteremshwa baharini pamoja na kuwepo kwa kampuni hiyo. Je, hufikaje Zanzibar kutoka Baharini?

(b) Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba Zanzibar inapata mapato kwa njia ya vipali, wakala na kodi. Ningeomba kujua je, kwa mwaka uliopita Zanzibar tulipata shilingi ngapi katika mfuko wa serikali.

(c) Hivi uwamuzi wa serikali wa kuamua kuhaulisha mafuta baharini, hatuoni kwamba kuna mwanya mzuri wa kuwafanya watu wa magendo kuuza mafuta.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba swali la (a) na (c) Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali (a) na (c) ni:

(a) Naomba kujua baada ya mafuta kuhaulishwa baharini kwa kupitia kampuni muliyoiteuwa hufikaje hapa kwenye ardhi yetu ya Zanzibar ni kwa kupitia chombo gani, hiyo kampuni hutufikishiaje mafuta hapa juu.

(c) Hivi uwamuzi wenu wa kuamua kusafirisha mafuta baharini, je hamtowi mwanya kwa watu wa magendo kuuza mafuta hayo kiholela?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, pamoja na kurudia swali lake la (a) sikulipata, ila swali lake la (c) nimelipata. Mhe. Spika, swali lake moja lilihusiana na mapato yanayopatikana serikalini.

Mhe. Spika: Hebu rudia tena kwa utulivu kabisa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize maswali yote matatu ili ayapate kwa vizuri zaidi.

(a) Mafuta hufikaje hapa Zanzibar kutoka baharini?

(b) Nilitaka kujua kwamba kwa mwaka jana kwa kupitia kibali, wakala na kodi ya TRA. Je, Zanzibar tulipata shilingi ngapi?

(c) Je, fursa hii ambayo serikali imeitoa ya kuhaulisha mafuta baharini, haitowi mwanya kwa watu wa rushwa au watu wa magendo kufanya biashara ya mafuta baharini?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru. Mhe. Spika, imeelezwa katika jibu mama kwamba biashara hii ni halali na uhalali wake unazidi kwamba wakati wanafanya hii shift to shift, mafuta kutoka meli hii kuingizwa meli nyengine, kuna vyombo vya serikali vinavyoshuhudia. Kwa hivyo, hapa hakuna uharamia wala hakuna magendo.

(a) Lakini mafuta yanafikaje huku kwetu. Kwanza asifikiri kwamba meli zinazofanya hiyo transfer ni meli zetu, inawezekana ni meli zetu na inawezekana sio meli zetu. Lakini ni meli katika uwanja wa bahari. Hii ni International Business inafanywa sio hapa kwetu tu, lakini na kwengine kokote. Hapa kwetu wanapapenda sana tu kwa sababu bahari muda wote ni tulivu na halafu inafanywa karibu na mji, sio kwamba inafanywa miles and miles ndani ya bahari off shore. Kwa hivyo, hata kama kuna kitu cha kuokoa mara moja basi ni rahisi.

(b) Ni kiasi gani serikali inapata kama mapato. Wizara yangu ina mapato ya aina mbili kama nilivyosema na yote ni mapato ya serikali. Mapato ya kibali kama aliyosema ambayo kwa mwaka 2009/2010 mamlaka ya usalama wa bahari, Zanzibar Maritime Authority wamepata dola 18,000. Hii utaiona ni ndogo, lakini vibali vinatolewa kwa mujibu wa gross tanager na tuna charge sent 8 za Kimarekani kwa gross tanager moja.

Lakini Shirika la Meli na Uwakala limepata dola za Kimarekani 200,002,818.8.TRA hatuna taarifa zao. Lakini swali la (c), limejibiwa na swali (a) kwamba hakuna uharamia. Kwa hivyo, hakuna kitu ambacho kinaweza kikafanyika kama magendo katika kufanya biashara hii. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, naomba kidogo kutoa maelezo ya ziada ili Mhe. Mwakilishi aweze kuwa na upeo na ufahamu mzuri wa hili suala.

Mhe. Spika, kwanza ni lazima tufahamu kwamba mafuta mengi yanapatikana katika nchi za Huba na sio kila nchi ina uwezo wa kununua mafuta kwa wingi. Kuna nchi zetu ndogo ndogo huwa tunanunua mafuta kulingana na mahitaji yetu. Biashara hii inazisaidia sana nchi ndogo ndogo, kwa maana ya kwamba meli inayopita inakuwa ni kubwa na inakuwa na mafuta mengi. Kwa hivyo,

nyinyi mnapohitajia mafuta kidogo kwa mujibu wa matumizi yenu, basi mnafanya mawasiliano ile meli inakaa nje halafu meli zenu ndogo zinakwenda na kupakia idadi mnayohitajia halafu ina-*anchor* katika bandari zenu. Hii itatusaidia ile kwa Kiingereza inaitwa *economy of scales*. Kwa maana ya kwamba kunakuwa kuna bilk *procurement,* mafuta yanakuja kwa wingi, nyinyi mnapewa ile sehemu yenu mnayohitajia.

Kwa upande wa Zanzibar sisi kama tunahitajia sehemu ile ndio tunayokwenda tukanunua na sisi tukaileta katika bandari yetu, na pale ndipo ambapo kile kima kinachoingia ndani, ndio kima kile kinachopaswa kutozwa kodi. Lakini kwa utaratibu wetu sisi huwa hatuna *classification* ni mafuta ya aina gani ambayo tumeyachukua kule. Sisi tukiingia ndani mzigo ulioingia ndani kwa umoja wake ndio tunaoutoza kodi.

Kwa hivyo, *specification* hiyo anayoitaka kwa maana kwamba meli zilizokaa nje na mafuta yaliyoingia ndani ni kodi kiasi gani tuliyopata, specification hiyo nadhani atashindwa kuipata kwetu. Sisi *clacification* ambayo tuliyonayo ni kwamba kodi yote ya mafuta tunatoa kiasi gani.

Nam. 64

Ajali Zinazosababishwa na Uzembe wa Madereva

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wananchi dhidi ya madereva wa daladala na magari ya shamba wanaoendesha gari kwa mwendo wa kasi na kukiuka sheria za Usalama Barabarani, na kusababisha ajali.

(a) Je, Mhe. Waziri ni ajali ngapi zilizosababishwa na dala dala, Zanzibar kwa mwaka 2009/2010.

(b) Je, Serikali inachukua hatua zipi kwa madereva wa aina hiyo ili kukomesha mtindo huu ambao kwa sasa unaonekana umeota mizizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wananchi dhidi ya madereva wa daladala na magari ya shamba ambao wanaendesha gari kwa mwendo wa kasi na kukiuka sheria za usalama barabarani na kusababisha ajali.

(a) Kuanzia Januari 2009 hadi Disemba 2010 katika visiwa vya Zanzibar zilitokezea jumla ya ajali 1504 za barabarani. Aidha, katika ajali hizo jumla ya ajali 387 zilisababishwa na madereva wa magari ya daladala na magari ya shamba. Idadi hizo ni wastani wa asilimia 25.73 ya ajali zote.

(b) Ili kukomesha mtindo huu ambao kwa sasa unaonekana umeota mizizi Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Utaratibu wa kupata leseni za kuendesha magari ya abiria zinatolewa kwa madereva waliotimia umri wa miaka 25, madereva ambao wanauzoefu wa kuendesha magari ya kawaida yasiokuwa ya abiria kwa muda usiopungua miaka miwili.

(ii) Wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inatumia kipimo cha kupimia mwendokasi wa gari ili kuyadhibiti magari yote yanayokwenda kwa mwendokasi zaidi ya ule uliokubalika kisheria.

(iii) Madereva wote waliokamatwa kwa makosa hayo wamefikishwa Mahakamani.

Aidha katika kutimiza hilo wizara yangu kwa kupitia Idara ya Usafiri na Leseni imeshazifuta leseni tano (5) na leseni kumi na tano (15) kuzifungia kwa muda wa miaka miwili. Madereva watano (5) kati ya hao wamefutiwa leseni zao na hawatapewa leseni tena mpya hadi baada ya kipindi cha mwaka mmoja kwa kufuata taratibu zote za uombaji wa leseni mpya.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri hivi sasa barabara ya Amani Dunga inafanyiwa matengenezo makubwa. Je, wizara yako imejipanga vipi katika kuchukua tahadhari ya kupunguza ajali, hasa tukizingatia kwamba barabara hii inatumika kwa magari mengi, yakiwemo magari ya abiria ya kwenda shamba pamoja na magari ya daladala na magari ya binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha ujenzi wa barabara kina taratibu zake na tunazitambua, namna ya utumiaji wa barabara katika kipindi cha ujenzi makampuni yanayojenga huwa yanaandaa vijana wanaoelekeza namna ya kupita ili matumizi ya barabara yasikwamishe utaratibu wa barabara unaoendelea. Naamini utaratibu uliopo ni mzuri na tunaomba tu kwamba Mhe. Mwakilishi tuwashajihishe

madereva wetu wawe waangalifu na wenye kufuata taratibu na maelekezo wanayopewa na vijana wahusika.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kumekuwa na tatizo la daladala za Bububu kutokufika Hospitali ya Mnazi Mmoja, wakati route zinaonesha kuishia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa hivyo wanasababisha usumbufu kwa wananchi hasa wagonjwa. Swali.

Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mpango gani kuhusu madereva wanaovunja sheria?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika jibu mama tumeeleza namna madereva wanavyovunja sheria na hatua zinazochukuliwa. Naomba tumuhakikishie Mhe. Mwakilishi kama kutakuwa kuna dereva ambaye unahisi anakiuka sheria na bado labda mkono wa serikali haujamfika, naomba tujulishe na ninakuhakikishia hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza dogo kama ifuatavyo. Kwa kuwa suala hili la kutokufuata sheria kunakopelekea malalamiko mengi kutokana na matumizi ya daladala na magari ya aina hii na kwa kuwa mji wetu sasa umekuwa sana.

Je, Mhe. Spika, wizara haioni haja sasa ya kuwa na utaratibu wa kuwa na mabasi ya kisasa ambayo yatakuwa yanahudumia mji wetu kama miji mingine, ili mji wetu uweze kuepuka ajali hizi lakini pia uweze kwenda sambamba na maendeleo ya ukuaji wa nchi yetu, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli mji wetu unaongezeka na huduma za usafiri nazo zinaongezaka. Nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kuwa na mabasi makubwa. Lakini kwa muda huu wizara yangu imetoa maelekezo, kwanza kuzidhibiti gari zote ndogo ndogo zenye kuchukua abiria 15 kuja chini. Katika kutimiza hilo, tumekusudia kwamba magari yote yenye uwezo wa kuchukua abiria 28 kwenda juu ndio yatakayotumika kwa huduma za daladala.

Mhe. Spika, mategemeo yetu hali itakaporuhusu tunayo haja na uwezekano wa kuweza kutumia mabasi ya kasi kutumika Zanzibar na itakuwa ni faraja. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar, 2011

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, jana tulikubaliana kwamba leo tufanye majumuisho. Kwa hivyo, nafasi ya kwanza nimpe Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya mwanzo asubuhi ya leo, ili na mimi niweze kuzungumza machache katika mswada huu uliowasilishwa na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria ya kuweka masharti ya uendelezaji, ukuzaji na uwekaji wa viwango na ubora wa bidhaa ni miongoni mwa miswada ambayo ni muhimu sana, hasa katika kipindi hiki ambacho tunakusudia Zanzibar yetu iingie katika masuala ya ushindani wa kibiashara.

Vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wangu wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa jinsi alivyowasilisha mswada ule kwa ustadi na uelewa mkubwa. Kutokana na hali hiyo, ndio maana Mhe. Spika sina shaka kabisa kwamba Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu wameweza kuuelewa na hatimaye kuuchangia bila ya kugugumizi au wamekuwa stadi katika kutoa mifano ambayo imetupa upeo mkubwa juu ya umuhimu wa mswada huu.

Kwa kweli kama tutajitoa kwa ajili ya kuufanyiakazi ipasavyo kama vile ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wameonesha wakati walipokuwa wakichangia kwamba wameukubali kidhati na kuufanyiakazi kwa umoja wetu. Kwa hivyo, hapana shaka Mhe. Spika lengo la Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuirejesha Zanzibar yetu haiba yake, yaani ya kuifanya iwe *Center for Excellency* katika masuala yote ya biashara kwa ujumla wake itafanikiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu ambao wameuchangia mswada huu walionesha kukerwa sana na mtindo ulioibuka hivi sasa hapa visiwani wa kuzalisha au kutengeneza ama kuingiza nchini bidhaa ambazo hazikidhi haja ama ziko chini ya viwango ambavyo havistahiki kutumika, yaani ni viwango ambavyo vinahitaji kufanyiwa marekebisho, ili twende na viwango vinavyokubalika.

Kwa kweli mifano mingi sana imetolewa tukianzia na bidhaa za vyakula. Tukiangalia vyakula tunavyonunua madukani ambavyo tayari vimeshapoteza

haiba yake pamoja na ubora wake. Vile vile bidhaa ambazo si za vyakula lakini ni bidhaa za matumizi ya kawaida na mifano imetolewa kama vile simu za mikononi, nyaya za umeme pamoja na vifaa vingi vya ujenzi vinaingizwa nchi na havina viwango vinavyokubalika.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu walionesha umuhimu wa kuweka mkazo zaidi bidhaa zile ambazo zinaleta athari ya moja kwa moja katika matumizi ya binadamu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili, kwamba katika mswada suala hili limezungumziwa na ndipo pale katika kipengele kilichomtaka Mhe. Waziri, yaani kutakuwa na viwango vya lazima kutumika.

Miongoni mwa sababu zilizopelekea kuweka kipengele hicho Mhe. Spika, kutokana na kuziona hizi bidhaa ambazo zinaleta athari au madhara moja kwa moja kwa mtumiaji ambazo hazifikii viwango vinavyokubalika, basi viwango hivyo ni lazima vitiliwe mkazo vitumike Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nawanaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kupitia kwako Mhe. Spika, watoe wasiwasi kuhusiana na suala hilo, kwa sababu tayari mswada huu umezingatia jambo hilo.

Mhe. Spika, pia napenda kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na suala zima la umuhimu wa kuzingatia, yaani tuwe waangalifu zaidi wakati tunapoangamiza bidhaa ambazo hazijafikia kiwango. Kwa kweli suala hili pia limezingatiwa kwenye mswada na ndio maana kuna taasisi nyingi ambazo zitahusishwa katika kufanikisha jambo hili.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeona umuhimu ya wote hayo na ndio maana tukawasilisha mswada huu hapa.

Kwa hiyo, tunachokiomba kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, ili mswada huu wa sheria uweze kupita basi tutahitaji mashirikiano ya pamoja ndani ya Baraza hili. Vile vile katika kuitekeleza sheria hii Mhe. Spika, basi tunahitaji mashirikiano ya hali ya juu na sio tu kwa taasisi za serikali, lakini pamoja na zile ambazo si za serikali.

Mhe. Spika, nikiendelea sasa naomba nizungumzie kuhusu suala zima la mashirikinao ambalo ni muhimu sana. Kwa kweli kuna jumuiya nyingi za kibinafsi nazo tutaziomba zitoe ushirikano wa hali ya juu katika kufanikisha hili, usimamizi kuna vyombo ambavyo vinahitaji vishirikishwe ipasavyo na tutaviomba navyo vitoe msukumo katika kusimamia sheria hii.

Kutokana na hali hiyo, kuna sheria nyingi sana ambazo tumezipitisha hapa Barazani, lakini udhaifu umejitokeza katika usimamizi wa sheria hizo. Kwa hivyo, tutawaomba wahusika wakuu waliotajwa katika sheria hii, basi tuwe nao katika mashirikiano na kuhakikisha kwamba kila ambalo tumelikusudia hapa linatekelezeka.

Mhe. Spika, nimeomba nitie baraka kidogo katika mswada huu, kwa sababu tayari katika utaratibu mzima wa kuandaa sheria hii nimeshiriki na hasa pale ambapo tulifikia kwenye ukamilishaji wa mswada huu wa sheria.

Nadhani mengi atayajumuisha Mhe. Waziri, lakini na mimi kama Wajumbe wa Baraza lako tukufu walivyouchangia kwa umoja wao, basi niendelee kuwaomba kwamba tuupitishe mswada huu kwa umoja wetu, ili uwe sheria. Sasa baada ya kuwa sheria tuendelee kushirikiana kwa umoja wetu katika kuona kuwa unafanyakazi iliyokusudiwa ya kuiondoa Zanzibar yetu kuwa jaa la bidhaa zisizokubalika na mlaji, isipokuwa tuifanye iwe Zanzibar mpya na kuwa Kivutio cha Biashara.

Mhe. Spika, na mimi niungane na Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kuungana mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa uwezo pamoja na ukaribu wake kwa kutujaalia kujadili mswada huu wetu kwa utulivu na mafanikio makubwa.

Vile vile Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukupongeza pamoja na kukushukuru kwa namna ulivyoongoza mjadala wa mswada huu kwa ustadi mkubwa na kiwango cha hali ya juu. Kwa kweli hii inaonesha dhahiri ukomavu wako kwenye nafasi hii na namna unavyokimudu Kiti cha Uspika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimefarajika sana kuwa waziri wa mwanzo kuwasilisha hoja katika Baraza la Nane la Wawakilishi pia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Awamu ya Saba. Kwa kweli hali hii inanipa moyo mkubwa wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kueleza yafuatayo:-

Naomba sasa kufanya majumuisho ya Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendelezaji, Ukuzaji na Uwekaji wa Viwango, Ubora wa Bidhaa na Usimamizi wa Huduma Zinazolingana na Hizo na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, tunaomba kuwashukuru kwa dhati wachangiaji wote waliochangia mswada huu. Idadi ya Waheshimiwa Wajumbe waliochangia mswada huu ni 31 Mhe. Spika, ambao wamechangia kwa ufasaha na umahiri mkubwa, michango ambayo ni mizigo waliyoitoa timeitia maanani na kuizingatia.

Vile vile naomba kumshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kunisaidia kufanya majumuisho Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba uniruhusu pia niwataje wachangiaji hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyeki wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo,
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman,
3. Mhe. Saleh Nassor Juma,
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub,
5. Mhe. Mohamoud Muhammed Mussa,
6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla,
7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis,
8. Mhe. Ali Abdalla Ali,
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu,
10. Mhe. Abdalla Moh'd Ali,
11. Mhe. Raya Suleiman Hamad,
12. Mhe. Ali Salum Haji,
13. Mhe. Bikame Yussuf Hamad,
14. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi,
15. Mhe. Hamza Hassan Juma,
16. Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiye na Wizara Maalum),
17. Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum),
18. Mhe. Salim Abdalla Hamad,
19. Mhe. Salma Mohammed Ali,
20. Mhe. Hassan Hamad Omar,
21. Mhe. Asha Abdu Haji,
22. Mhe. Waziri wa Afya,
23. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa,
24. Mhe. Fatma Mbarouk Said,
25. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman,
26. Mhe. Hija Hassan Hija,
27. Mhe. Subeit Khamis Faki,
28. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi,
29. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk,
30. Mhe. Mohammed Haji Khalid, na

31. Ussi Jecha Simai ambaye amewasilisha mchango wake kwa maandishi. (Makofi)

Mhe. Spika, kwanza kabisa tunamshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa miongozo mizuri aliyotupa katika hotuba yake aliyoitoa na tunaahidi kuwa tutaifanyiakazi yote, ili kuweka mazingira mazuri ya kuitendaji wa sheria hii.
Vile vile tunapenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba hapatakuwa na migongano baina ya taasisi zetu za Wizara ya Afya na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kutekeleza majukumu yetu, isipokuwa sheria hii itatoa fursa na nguvu mpya ya mashirikiano katika kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Wazanzibari wote. (Makofi)

Mhe. Spika, sote tunaamini kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali ni kitengo muhimu sana na kwamba ni taasisi ya rufaa na maamuzi ya mwisho kwa masuala ya uchunguzi nchini.

Hata hivyo, tunayo furaha kubwa kuwa Wizara ya Afya inatayarisha mswada wa sheria kuhusu Afisi ya Mkemia Mkuu na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko itashirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa vifaa vinavyotumika kwa Mkemia Mkuu vinafikia viwango vya lazima, ili kukidhi matakwa ya sheria hiyo.

Mwisho tunamshukuru Mwenyekiti pamoja na kamati yake yote kwa kuunga mkono hoja yetu hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu kuchelewa kuwafika kwa wakati mswada huu Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu. Kwa kweli tunasikitika sana kwa kuchelewa kuwafika mswada huu ambapo unatakiwa ufike siku 21. Hata hivyo, hali hiyo ilijitokeza kutokana na sababu za kiufundi na tunaomba radhi kwa hali hiyo iliyojitokeza.

Kwa ujumla tumepata mawazo na mapendekezo mbali mbali kuhusu tafsiri ya maneno pamoja na tofauti ya tafsiri za mswada ulioandikwa kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha maswali mengi ya baadhi ya Wajumbe wanaosema, ambao wametoa ufafanuzi mzuri na mpana kujibu baadhi ya maswali ya Wajumbe.

Kwa kweli tunawashukuru sana Wajumbe hao Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiye na Wizara Maalum), Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe hawa wamejitahidi sana wakati waliposimam na kutoa maelezo ya maswali

mengi ambayo yaliulizwa hapa, ambapo yamechangia sana kutusaidia kueleza Wajumbe kinaga ubaga hali gani ya mswada huu umuhimu wake.

Mhe. Spika, kuhusu tafsiri ya maneno yametokana na maudhui ya mswada wenyewe. Hata hivyo, wataalamu wayaangalia maneno hayo na kuyafanyiakazi kwa kadri hali inavyofaa na marekebisho yote yaliyofanywa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo yatatumiwa kikamilifu kwenye mswada huu.

Kuhusu kifungu Nam. 6 cha uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi kwa njia ya kutangaza nafasi hiyo. Mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ni mazuri na tunayachukua kama ni ushauri kwa serikali. Lakini kwa muda huu utaratibu ulioelezwa kwenye kipengele hiki ndio unaotumika katika kuwateua wakuu wa vyombo kama hivi vya kiserikali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunaamini kwamba Mhe. Rais atamteua mtendaji mkuu kulingana na sifa zilizoelezwa na atayefaa kwa shughuli hii.

Vile vile kuhusu kifungu cha 6 (4) tunaomba Waheshimiwa waelewe kwamba Mkurugenzi Mkuu anateuliwa na Rais na anapewa hadudirejea zinazomtaka kuwajibika kwa bodi. Kwa hivyo, tunaamini kwamba Mkurugenzi huyo atatekeleza majukumu yake yote kama ipasavyo kama hivi sasa bodi nyengine zinavyoendeshwa.

Katika kifungu cha 7 (2) tunaomba Waheshimiwa Wajumbe waondoe wasiwasi juu ya utekelezaji wa taasisi hii, kwani taasisi hii itakuwa na wajibu wa kupeleka matumizi yake kwa bodi na kupitishwa kulingana na matumizi waliyoyaweka, pia mahesabu yao yote yataangaliwa na kuchunguzwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kifungu cha 8 (5) kinachohusu masuala ya jaduweli. Kwa kweli jaduweli hili linaeleza mwenendo na vikao vya bodi ambalo linapitishwa na Baraza lako tukufu hii leo waziri kama ndiye kiongozi wa juu kwenye bodi hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anapewa mamlaka na Baraza hili tukufu kubadilisha, kurekebisha, kuondosha na kufuta jambo lolote kwenye jaduweli la sheria hii kupitia Gazeti Rasmi la Serikali baada ya kushauriana na watendaji wake na wala jambo hili halimpi waziri kuingilia utendaji wa bodi, isipokuwa ni mwenendo wa vikao vya bodi tu.

Tukiangalia kwenye kifungu cha. 6 (2) (c) na hapa Mhe. Spika, tunaomba kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Kwa kweli kifungu cha 36 cha sheria hii kinampa waziri uwezo wa kutunga kanuni za mambo ya jumla katika utekelezaji wa masharti na madhumuni ya sheria hii. Hivyo, kwa yale yote mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameshauri,

basi yatazingatiwa kwa kadri itakavyoonekana inafaa na kutumiwa katika utengenezaji wa kanuni hizo.

Pia kifungu cha 20 (1) taratibu za kisheria zinaelekeza kwamba kama mhusika mkuu hatokuwepo basi wakala wake atabeba dhamana zote alizokuwa akiwajibika nazo.

Katika kifungu cha 20 (6) kimewekwa kwa makusudi, ili kunusuru uharibifu wa mazingira na afya kwa wananchi wetu pamoja na kuwasaidia wafanyabiashara kudai haki zao pale wanapodhulumiwa.

Mhe. Spika, naomba kufupisha kwamba mchele uliokwenda Pemba sio mchele uliorudishwa kule Pakistani, kwani mchele huo uliorudishwa Pakistani ulikuwa na aina fulani ya sumu ijulikanayo kama Organic Phosphorus na mchele huo ulisafirishwa kutoka hapa na kurejeshwa nchini Pakistani. Kwa maana hiyo, mchele uliokwenda Pemba ulichunguzwa na wala haukuwa na sumu ya aina yoyote.

Mhe. Mohammed Haji Khalid ameeleza hasara ya uharibufu wa bidhaa kama hizo kwa mazingira ya nchi na afya za wananchi pindi bidhaa nyengine zenye sumu zikiteketezwa nchini zinaweza kuleta madhara makubwa zaidi katika nchi yetu. Bidhaa nyengine zenye sumu zikifukiwa kwenye ardhi sumu ile itatembea na kwenda kwenye visima vyetu vya maji, kwa upande wa bahari samaki wataila na baadaye samaki tutawala wenyewe. Kutokana na hali hiyo, bidhaa nyengine zinahitaji zirejeshwe zilikotoka.

Mhe. Spika, *Zanzibar Bureau Standard (ZBS)* ni taasisi itakayoweka viwango vya bidhaa zote zitakazoingia na kuzalishwa nchini pamoja na huduma zitakazotolewa hapa nchini. Kwa kweli tunaamini kwamba Zanzibar haitokuwa tena jaa la bidhaa mbovu na badala yake visiwa hivi vitabeba sifa na kutambulika rasmi na kuwaita wateja wengi sana kuja kwa ajili ya kufanya biashara visiwani Zanzibar kutokana na sifa ya kuwa na bidhaa safi, nzuri na zenye viwango bora. (*Makofi*)

Zanzibar Bureau Standard (ZBS) itashirikiana na Tanzania Bureau Standard (TBS) na taasisi za viwango za Kikanda, kama vile Afrika ya Mashariki, SADC na za Kimataifa kuona bidhaa za Zanzibar zinapata soko la uhakika katika maeneo yote hayo pamoja na kuimarisha ushirikiano huo, ili mradi inafuata sheria ipasavyo.

Mhe. Spika, suala la kuweka viwango vya bidhaa litashajihisha na kuimarisha shughuli za viwanda, ambazo zitashajihisha vile vile kuongeza ajira kwa wananchi wetu. Sambamba na hilo zitasaidia wananchi kiafya na kiuchumi kwa

vile watanunua bidhaa zenye ubora na zenye kudumu na hiyo itapunguza umasikuni kwa hali ya juu katika nchi yetu.

Nikiendelea sasa nizungumzie kuhusu mjumbe mmoja wa bodi kutoka katika Sekta ya Kilimo. Mjumbe mmoja katika bodi hii atatoka kwenye Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenyeviwanda na Wakulima. Kwa hivyo, mjumbe huyu ndiye atakayewawakilishi wafanyabiashara na wakulima kutoka katika Jumuiya yao ya Wafanyabiashara Wenyeviwanda na Wakulima kama jumuiya hiyo ilivyoundwa.

Kuhusu kifungu cha 26 (1) kinatoa adhabu kulingana na makosa ya kwenda kinyume ya masharti ya sheria hii. Mhe. Spika, tunakubaliana na msemo wa Waheshimiwa Wajumbe kwamba bidhaa bora ni afya bora. Kwa hivyo, wizara yetu kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika itafanyakazi kubwa ya kuelimisha na kuwafundisha wafanyabiashara pamoja na wananchi wote, maudhui na umuhimu wa sheria hii na itashajihisha wananchi kuzalisha bidhaa zilizobora kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini.

Mhe. Spika, wajumbe wengi wametaka kujua kuhusu mchele wa mapembe. Kwa kweli suala hili limeelezwa vizuri na Mhe. Hamza Hassan Juma na tunamshukuru na tunampongeza sana kwa hilo. Sasa suala tunalolizungumzia sisi ni bidhaa au vyakula ama huduma iliyochini ya viwango na sio chapa wala alama ya bidhaa au chakula ama huduma. (*Makofi*)

Vile vile kuhusu suala la unyonge au umasikini utaongezeka zaidi ni pale ambapo mteja atakapopewa huduma duni kwa bei kubwa au akapewa chakula kisichofaa kwa bei isiyofaa. Kwa hiyo, umasikini utaongezeka zaidi anapokwenda kununua chakula kilichochini ya viwango. Kutokana na hali hiyo, tunawaomba wananchi washirikiane na serikali yao kutokomeza bidhaa zisizo na viwango kwa kutoa taarifa sahihi pindipo wakigundua suala hilo linatendeka hasa kwa kupitia njia zisizokubalika, kugomea kabisa kununua bidhaa ambazo ziko chini ya viwango au bidhaa mbovu mashirikiano baina ya wananchi na taasisi zetu zitasaidia sana kuondosha suala hili kwa haraka.

Mhe. Spika, kuna wafanya biashara ambao huenda nchini China kutengeneza bidhaa au vifaa vyenye viwango duni kwa kutumia majina makubwa makubwa na kuja kuuza bidhaa hizo hapa Zanzibar kwa bei kubwa, wakati hakukutimia viwango.

Mhe. Spika, kuna wafanya biashara hapa Zanzibar wasio waaminifu wanatengeneza tomato wakazitia katika mageleni kwa kutumia unga wa ngano rangi na ndimu ya unga, na ikafanywa tomato na ikatumiwa na wananchi wetu hapa hapa Zanzibar.

Kuna wengine hutengeneza Jic kwa kutumia kamikeli kali na kufanya ndio dawa ya kuondolea madowa, mambo yamezidi kuna watu wanapita katika hoteli za kitalii wakakusanya mabaki ya mafuta yote yanayotumiwa katika mahoteli hayo kuyachuja na kuwauzia wauza chips, kukaangia chips na kuuza kiholola katika mitaa. Mafuta haya ni mchanganyiko wa mafuta mbali mbali mpaka mafuta ya nguruwe yamo ndani yake.

Mhe. Spika, haya yanafanyika humu humu ndani ya nchi yetu ndani ya kisiwa chetu jambo ambalo kwamba huhatarisha afya za wananchi, kwa sheria hii itakomesha mambo kama haya, mambo haya hayana budi kupigwa vita yasiendelee katika nchi yetu kwani yataweza kutupeleka pahala pabaya kabisa.

Mhe. Spika, kutokana na michango madhubuti ya wajumbe wa Baraza lako tukufu hasa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa tumeshawishika kubadilisha kifungu namba kumi na saba 17 sehemu ya viwango vya Zanzibar na kuweka viwango vya taifa national standard . Sheria hiyo ya viwango haitosababisha kufuta kwa sheria ya kumlinda mtumiaji kama baadhi ya wajumbe wetu walivyokuwa na wasi wasi, kwani hizi ni sheria mbili tofauti, moja inasimamia viwango hii ya ZBS na moja inasimamia ushindani na mwenendo mzima wa kibiashara. Kwa hivyo nataka tuwaondoe wasi wasi kabisa waheshimiwa wajumbe kwamba sheria hizi hazitogongana bali tutashirikiana na kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa kwa kuleta maendeleo ya Mzanzibari.

Mhe. Spika, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko katika kusimamia utekelezaji wa sheria hii tumedhamiria kuunda taasisi madhubuti itakayosimamia masharti ya uendelezaji, ukuzaji na usimamizi wa viwango na ubora wa bidhaa kwa kujenga majengo ya kisasa, kuwasomesha wataalam wake kwa ujuzi wa hali ya juu na kuweka maabara yenye dhana na vifaa vya kisasa vitakavyoweza kufanya kazi kwa ufanisimkubwa wa kufikia viwango vya kimataifa.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba wachangiaji wote walikuwa na nia thabiti ya kurutubisha mswada huu ili uwe na nguvu na uweze kutumika na kuleta tija na matarajio yaliyokusudiwa ya kuinua viwango vya bidhaa zinazozalishwa na zinazoingizwa hapa nchini, ili kurudisha haiba na hadhi ya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara katika kanda ya Afrika ya Mashariki na Kati.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo yote naomba kutoa hoja. Ahsante sana (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa maelezo yako na waheshimiwa wajumbe kwa kuunga mkono hoja yako.

Sasa itabidi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya Baraza zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

SEHEMU YA KWANZA PAMONA NA MAREKEBISHO YAKE

Kifungu cha Kwanza	-	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha Pili	-	Matumizi pamoja na maekebisho yake
Kifungu cha Tatu	-	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA PILI

UANZISHWAJI KAZI NA UONGOZI WA TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR PAMOJA NA MAREKEBISHO YAKE

Kifungu cha Tano	-	Kazi za Taasisi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Sita	-	Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu
Kifungu cha Saba	-	Uteuzi wa wafanyakazi wa taasisi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Nane	-	Bodi ya Wakurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Tisa	-	Muda wa Wajumbe wa Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi	-	Uwezo na Wajibu wa Bodi pamoja watumishi wake.

Kifungu cha Kumi na moja	-	Kamati za bodi.
Kifungu cha Kumi na Mbili	-	Alama za viwango pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Kumi na Tatu	-	Maombi ya kutumia alama ya viwango pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Nne	-	Rufaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Kumi na Tano	-	Sampuli vifaa na taarifa pamoja na Marekebisho yajke
KIfungu cha kumi na Sita	-	Viwango vya lazima pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha Kumi na Saba	-	Viwango vya Zanzibar pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Nane	-	Masharti juu ya Matumizi ya neno Kiwango pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Tisa	-	Bidhaa zisizokuwa na kiwango pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini	-	Ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha ishirini na Moja	-	Uteuzi wa Mkaguzi na Viwango pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na mbili	-	Uwezo wa Mkaguzi wa viwango pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na Tatu	-	Kufanya kosa na chombo kinachojitegemea pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na Nne	-	Uwajibikaji kwa mwajiri au wakala

Kifungu cha Ishirini na Tano	-	Kumaliza kosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na Sita	-	Adhabu ya jumla pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na Saba	-	Chanzo cha Fedha pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na Nane	-	Matumizi ya fedha pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini na Tisa	-	Bajeti ya mwaka na ya ziada Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Thalathini	-	Mkaguzi wa Fedha pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha thalathini na moja	-	Taarifa ya Mwaka ya Mkurugenzi Mkuu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Thalathini na mbili	-	Waziri kutoa maelekezo ya jumla Kwa bodi.
Kifungu cha Thalathini na tatu	-	Alama ya Viwango Kutolalamikiwa Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Thalathini na Nne	-	Kinga kwa bodi au Afisa wa Taasisi.
Kifungu cha Thalathini na Tano	-	Kutoa taarifa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Thalathini na Sita	-	Kanuni pamoja na marekebisho Yake.
Kifungu cha Thalathini na Saba	-	Masharti ya Mpito.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ilivyokuwa kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu kifungu baasa ya kifungu na

kuukubali bila ya mabadiliko yoyote pamoja na masahihisho. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho mbali mbali wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mswada wa Sheria wa Viwango ya Zanzibar 2011

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar 2011 usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Sasa nawahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Katibu anasema shughuli tulizopangiwa leo zimemalizika lakini naomba nitoe taarifa moja ndogo ya semina ambayo ni ya ZANTEL ya tarehe 29/01/2011, nilipokea taarifa kutoka kwa baadhi ya waheshimiwa Mawaziri kwamba tarehe 29/01/2011 siku ambayo tumeipanga kuwa na semina ya ZANTEL itakuwa sehemu fulani shambani huko siku hiyo waheshimiwa Mawaziri watakuwa na dharura tulikuwa tunajaribu kuwasiliana na ndugu zetu wa ZANTEL kama wajumbe mtakubali semina ile iweze kuitishwa siju ya jumapili badala yake ili wajumbe sote tuweze kushiriki katika semina ile.

Shirika la ZANTEL kama tunavyoelewa ni shirika letu na muhimu serikali ikaelewa kile kinachoendelea na pia serikali ikaelewa vile vile yale maelezo au mchango wa Waheshimiwa Wajumbe ili serikali iweze kusaidiana na Shirika la ZANTEL kutatua baadyi ya mambo ambayo waheshimiwa wajumbe wataweza kuuliza katika semina hiyo. Sasa nataka niwaambie tu kwamba hilo tunalifanyia kazi lakini hatujapata majibu. Jana tu ndio nimepata hiyo taarifa kwamba siku hiyo ya Jumamosi waheshimiwa Mawaziri watakuwa na shughuli nyengine muhimu ambayo itatufanya tubadilishe tarehe ya semina.

Kwa hivyo tunawasiliana na wenzetu wa ZANTEL tunategemea watakubali hivyo, ili kuweza kuita semina hiyo siku ya Jumapili badala ya Jumamosi. La muhimu kuweza kukumbuka kwamba shughuli zetu tunategemea kumaliza tarehe 28/01/2011 Mungu akipenda.

Sasa tulitaka tuiwahi siku ya Jumamosi ile ili tusije tukaweka waheshimiwa wajumbe hapa kwa muda mrefu bila ya kuzingatia maslahi yao. Lakini kwa sababu ya dharura hii tunataka kuwasilisha kwenu tuwaombe waheshimiwa wajumbe, kwa sababu nyote tunawahitaji muwepo. Wakubali tuwalaze siku ya Jumamosi bila ya kuwa na chochote. Hilo liko nje ya uwezo wetu wa bajeti, ili yote mawili tuweze kuyashughulikia. Kwa sababu semina ni muhimu na ilikuwa ni ahadi ya muda mrefu kwamba watafanya semina hiyo.

Lakini pia kwa dharura muhimu ya Mhe. Waziri ya kutomudu kushiriki kwenye semina hiyo siku ya Jumamosi kwa sababu ya shughuli nyengine, ndio tunaomba wenzetu wakubali wafanye siku ya Jumapili. Lakini pia Waheshimiwa Wajumbe tukubali siku ya Jumamosi ile ambayo itabidi tuwe tunangojea bila ya kwenda katika maeneo yetu basi tukubali kustahamili bila ya kuwa na msaada wowote. Kwa maneno mengine ambayo makofi haya yanathibitisha kukubali hivyo kwa maneno mengine tujitegemee. Ahsante sana.

Masuala mengine ambayo yamewasilishwa na wajumbe kutoka kwa Waziri tunayashughulikia haina haja ya kuyataja lakini tunayafanyia kazi.

(Saa 5:48 Asubuhi Baraza liliahirishwa hadi kesho tarehe 26/01/2011 Saa. 3.00 asubuhi).